

# MAOFISA WA MLANGONI KWAKO...

## USIWARUHUS U WAINGIE BILA WARANTI

Sawa na walivyo maafisa wa polisi, maafisa wa uhamiaji **hawawezi** kuingia kwako bila waranti iliyotiwa saini na jaji.

- **Usiwahi** kufungua mlango
- **Waombe** wapitisha waranti chini ya mlango au isimamishwe kwenye dirisha
- **Thibitisha** kwamba waranti ina jina **lako**
- Hata kama maafisa wa uhamiaji wana waranti, kama lina jina la mtu usiyemjua au mtu aliyekuwa akiishi kwako, **hawawezi** kuitumia kuingia kwako



### Ikiwa **hawana** waranti

Ikiwa maafisa wa Uhamiaji hawana waranti au ikiwa waranti ni ya mtu mwingine usiyemjua au mtu asiyeishi kwako, **waambie kwamba huwezi kuwaruhusu waingie bila kibali, au kwamba mtu wanayemtafuta haishi kwako, waombe kwa unyenyekevu kuondoka.**

Ikiwa wanamtafuta mtu unayemjua, huna haja ya kuwaambia mahali mtu huyo yuko, waambie wakupe anwani ya kuwasiliana nao, kisha uwaombe waondoke.

### Ikiwa **wana** waranti

Hata kama maafisa wa uhamiaji wana waranti, **bado una haki zako!**

Usiwaambie chochote, sema:

**“NIMEAMUA  
KUTUMIA  
MAREKEBISHO YA  
TANO YA SHERIA  
NA NINA HAKI YA  
KUWA KIMYA.”**

- **Endelea kusema hivyo** wakiamua kukupuuza.
- **Usisaini** hati zozote walizo nazo. Ni vyema kushauriwa na wakili kila wakati kama ni sawa kutia saini hati yoyote.
- **Usiwape** maafisa wa Uhamiaji hati yoyote inayokutambulisha kutoka nchi yako kama vile pasipoti yako.

### Ikiwa watakukamata wewe au watu wengine

Ikiwa maafisa wa Uhamiaji wana waranti na wakakukamata wewe au watu wengine kwako, **usitie hati yoyote saini wala kukubali jambo lolote.**

- **Kaa na namba** ya simu ya wakili unayeweza kumpigia.
- Hakikisha umeficha **namba na hati muhimu sehemu salama nyumbani kwako** ambapo wanafamilia au marafiki wanaweza kuzipata ili kukusaidia.

### rekodi mawasiliano yenu


Hakikisha mtu mwingine aliye nawe nyumbani anarekodi matukio kwa video au sauti akitumia simu au kifaa kingine. Maofisa wa Uhamiaji wanapoondoka, wewe au mwenzako anaweza kuandika kila kitu anachokumbuka: maafisa wa Uhamiaji walivyokuwa wamevalia, gari walilokuwa nalo, kilichotokea.

### ripoti hali ilivyokuwa

Ripoti mara moja kwamba maafisa wa Uhamiaji walikuja kwako.

Kama unaishi katika Jiji la New York, piga simu kwa Asasi ya Kulinda Wahamiaji (Immigrant Defense Project):  
**212-725-6422**

Kama unaishi nje ya Jiji la New York, piga simu kwa United We Dream:  
**1-844-363-1423**



# MAOFISA WA BARABARANI...

## waulize kama unaweza kwenda

Maofisa wa Uhamiaji wakikusimamisha barabarani na kukuuliza maswali, waulize moja kwa moja kama unaweza kwenda.

Wakikuambia ndiyo, waambie hutaki kujibu maswali yao na [uendeleo kuenda](#).

Wakisema huwezi kwenda, waambie:

**“NIMEAMUA KUTUMIA MAREKEBISHO YA TANO YA SHERIA NA NINA HAKI YA KUWA KIMYA.”**

## usikubali kukaguliwa

Usiruhusu maofisa wa Uhamiaji wakague vitu vyako au mifuko yako.

Waambie:

**“SIJAKUBALI UKAGUZI HUU.”**

## usijibu maswali

Usijibu maswali kuhusu hali yako ya uhamiaji au mahali nchi ulikotoka.

Waambie una [haki ya kuwa kimya](#).

## usiwaonyeshe hati zako

Usiwape hati zozote zinazoweza kukutambulisha kutoka nchini mwako (kwa mfano pasipoti yako).

## ripoti ulichoshuhudia

Ripoti moja kwa moja kwamba maofisa wa Uhamiaji walikusimamisha.

Kama unaishi katika Jiji la New York, piga simu kwa Asasi ya Kulinda Wahamiaji (Immigrant Defense Project):

**212-725-6422**

Kama unaishi nje ya Jiji la New York, piga simu kwa United We Dream:

**1-844-363-1423**


Kusimamishwa na maofisa wa Uhamiaji kunaweza kuhofisha sana, [lakini usikimbie](#) au kutoroka, [usiwape hati za uongo](#) na usiseme [uongo kamwe!](#)



# UKISHUHUDIA MAOFISA WA UHAMIAJI WAKIMSHIKA MTU AU WAKIMVAMIA...

## rekodi tukio hilo

Una haki ya kupiga picha na kurekodi tukio hilo. Fanya hivyo kutoka umbali salama ili usifanye hali ya kukamatwa au kuvamiwa kuwa mbaya.



## nakili

Andika

- ni maofisa wangapi wamehusika
- namba za beji zao (kama unaweza kuona)
- mavazi yao na kile kilichoandikwa kwenye sare au vesti zao
- gari walilokuwa nalo (pamoja na namba ya usajili).

## ripoti ulichoshuhudia

Ripoti ulichoshuhudia moja kwa moja!

Kama unaishi katika Jiji la New York, piga simu kwa Asasi ya Kulinda Wahamiaji (Immigrant Defense Project):

**212-725-6422**

Kama unaishi nje ya Jiji la New York, piga simu kwa United We Dream:

**1-844-363-1423**